

Pambazuko

Ukweli Hauna Kutu

Toleo Namba 007

Jumatatu Agosti 22-28, 2022

YALIYOMO:

UK. 4

Tozo yaibua
mnyukano wa
Nape, wananchi

UK.6

Hatutaki utalii
wa ngono

UK. 9

Sababu za anguko
la Raila, ushindi
wa Ruto



Tanzania yadhibiti magaidi

● *Matajiri Ulaya waongeza fedha Msumbiji*

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Maumivu ya tozo yapunguzwe

KUMEKUWEPO na kilio cha maumivu ya ugumu wa maisha kutoka kwa idadi kubwa ya wananchi. Siyo wa mijini tu, bali hata kutoka maeneo ya vijijini nako wanalia kupanda kwa gharama za maisha kila uchao.

Zipo sababu nyingi zinazotolewa na kila mmoja; wapo wanaodai ni kutokana na kuwepo kwa mfumuko mkubwa wa bei kwa bidhaa na huduma. Wapo pia wanaodai ni mbinu chafu za kujiongeza mapato kutoka kwa wafanyabiashara na wapo wanaolaumu serikali.

Serikali nayo kwa upande wake inaeleza wazi kwamba kuwepo kwa janga la ugonjwa uliosumbua zaidi duniani - Covid-19 kumechangia kwa kiasi kikubwa kupanda kwa gharama za maisha - kwani katika kipindi cha karibu miaka miwili, kuuza na kuagiza bidhaa kutoka nje ya Tanzania ilikuwa vigumu mno kutokana na masharti ya kukabili janga hilo.

Pia serikali inaeleza kuwepo kwa vita vya Russia na Ukraine kumeongeza zaidi bei ya bidhaa, hasa mafuta ambayo huagizwa kutoka nje. Pia bei ya vyakula, hasa ngano na mafuta ya kupikia, yanayotoka kwa wingi nchi za Bara la Asia, ilipanda kwani nchi za bara hilo, ikiwamo hizo zinazopigana, zilisitisha ama kupunguza kusafirisha bidhaa hizo kuja Afrika na maeneo mengine, hivyo kusababisha bei ya bidhaa kupanda.

Pamoja na sababu zote hizo, ambazo kila upande unaweza kuwa na uzito wake - bila kujali ukweli na usahihi, sisi katika Pambazuko, tunaamini kwamba serikali yetu inaweza kutumia

“uwezo wake mkubwa” kuikabili hali hii. Kwamba ikapunguza kilio cha wananchi kuhusu ugumu wa maisha kutokana na tozo.

Katika mazingira yoyote, kuongeza tozo kunamuimiza zaidi mwananchi, hasa wakati huu ambako kuna hizo sababu - nyingi zikiwa nje ya uwezo wetu kuzidhibiti.

Ikumbukwe kwamba tangu Julai 15 mwaka 2021, watumaji na wapokeaji wa fedha kupitia simu za mkononi walianza kulipa kodi ya miamala, hatua ambayo haikulalamikiwa sana kwani gharama zake zilikuwa himilivu kwa watumiaji wa huduma hiyo.


Hata hivyo, wapo pia waliolalamika na kuhamia kwenye miamala ya kibenki ambapo hakukuwa na makato makubwa.

Lakini sasa nako kwenye “uchochoro” kumezibwa tangu Julai Mosi, 2022 baada ya Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, kupitia gazeti la Serikali Namba 478, kutangaza kuanza utekelezwaji wa kodi ya miamala ya fedha kupitia benki.

Sisi tunaamini kabisa kwamba serikali inachopaswa kufanya ni kupanua wigo wa kodi kwa kubuni vyanzo vipya na kudhibiti upotevu wa makusanyo katika vyanzo vya kimkakati ikiwamo Bandari, kampuni kubwa za uzalishaji, kada ya utalii na kwingineko.

Ni wakati sasa wa Rais Samia Suluhu Hassan kuonyesha kwamba anakwazwa na mlundikano wa kodi kwa mwananchi kwenye huduma na bidhaa muhimu katika kuendesha maisha ya kila siku.

Inawezekana.



Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno “**HABARI**” kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: pambazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno “**HABARI**” na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



TUNAWEZAJE hamasisha watu kuchangia maendeleo wakati kila mwaka wanaona ripoti za ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha ya umma? Nchi yetu haina tatizo la mapato, tuna shida kubwa ya matumizi. Tujirekebisha. - Rebecca Gyumi (mwanasheria na mteteki wa haki za wanawake. Ni mshindi wa tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu, 2018).

Tozo yaibua mnyukano wa Nape, wananchi

Na Tryruckia Mfinanga

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye amedhihirisha namna serikali inaweza kuvunja ukiritimba na ugumu wa kupata majibu ya serikali kuhusu kero na madhila mbalimbali.

Hili limedhihirika wiki iliyoisha jana, baada ya Nape kujibu maswali mengi juu ya ongezeko la kile kinachoitwa na wananchi – “tozo umiza.” Waziri huyo alitumia mtandao wa Twitter kueleza msimamo wa serikali na namna inavyoshughulikia malalamiko ya wananchi.

Hadi Pambazuko linaingia mtamboni kuchapishwa – saa 3:27 usiku jana, watu 211 walikuwa wakizunguma na Waziri Nape kuhusu ongezeko la tozo katika gharama za kununua vifurushi vya kujiunga na mawasiliano ya intaneti – maarufu bando.

Nape anasema; “Tanzania ni nchi ya sita kwa bei ndogo ya bando Afrika na ya 50 duniani tukitanguliwa na Algeria - wana 0.48, Libya 0.61, Ghana 0.61, Morocco halafu inafuatia Tanzania. Takwimu hizi siyo za Serikali ni za mashirika makubwa duniani.”

Waziri Nape anaendelea kueleza kwamba Tanzania ni miongoni mwa mataifa machache yenye gharama za chini za mawasiliano, ingawa hiyo haimaanishi kuwa itapunguza malalamiko kwa kuwa uchumi wan chi haufanani na wananchi wengi wana vipato vya chini.

Baada ya maelezo hayo, wananchi kupitia Twitter walianza kueleza wanachoamini kutokana na maelezo yake, huku wengi wakibainika kutofurahia alichokieleza Waziri huyo kwa niaba ya serikali.

Vicensia Shule (anayetumia anwani ya - @vicensiashule): anaandika; “Waziri unamdanganya nani. Unampotosha nani? Rais, Watanganyika kwa faida ya nani? Waziri unafikiri Watanganyika hawajui



Rais Samia Suluhu Hassan (Picha - Gazeti la Mwananchi).

hizo nchi unazozitaja? Waziri Nape huu siyo muda wa kucheza na hisia za watu. Tozo na makato ni makali mno kwa Watanganyika, Shauri kwa hekima.”

Nape akajibu (kwa maandishi ya herufi kubwa): “Acha kupotosha watu bila sababu. Takwimu hizo siyo za serikali, kama una takwimu tofauti weka hapa. Na wewe ni msomi, huwezi kuishi kwa maneno matupu, weka zako zinazoonyesha uongo wangu.”

Vicensia akaendelea; “Tujadili. Huwezi kusema mdumange ni ngoma bora au ya sita kwa ubora kuliko sindimba, mkwaju, mheme au lizombe kwa kuwa ngoma zote hizo zinatoka kwenye jamii na matumizi tofauti. Ni ulinganifu usilingana. Ni sawa kabisa na mazingira ya sasa ya tozo na ulinganifu unaofanya.”

Mwananchi mwingine anayejitua Mufadal Zober (@mufathegreat) anaandika; “kweli kabisa, nakuunga mkono. Halafu tunaambiwa eti uchumi wetu unaendelea kuimarika wakati tunaathirika kwa mfulumko wa bei mfululizo na kama wanasema kwamba uchumi wetu unaimarika, basi washushe bei.”

Rais anaweza kugawa pesa za maendeleo?

Na Dkt. Bullet Ruhinda

IMEKUWA jambo la kawaida kuwasikia viongozi karibu wote wa Serikali ya Tanzania na wale wa chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakitoa pongezi kwa rais wa nchi anayekuwa madarakani.

Hawa hueleza umma kwamba kiongozi wa nchi ametoa pesa nyingi katika shughuli kadhaa za kuleta maendeleo na kupunguza ukali wa maisha magumu kwa wananchi.

Sikumbuki kuwahi kumsikia rais yeyote wa Tanzania akisema “amepeleka pesa mahali,” bali husema serikali imepeleka pesa na mara nyingine husema “tumepeleka” kwa maana ya serikali.

Je nini chanzo cha tofauti hii? Je, ni makusudi au kuna ajenda nyuma ya mkanganyiko huo?

Iweje rais ajue kwamba yeye hana pesa, bali pesa ni za serikali (au wananchi), lakini viongozi na wateule wake hawajui hilo? Tukiacha hilo, je, wananchi wanajua kwamba pesa zinazotolewa kwa ajili ya maendeleo ni kodi zao? Je, wanajua kati yao na Rais nani anatoa pesa?

Kwa nini viongozi wengi wanasisitiza wananchi kulipa kodi kwa uaminifu, lakini mara nyingi hawaambiwi kwamba pesa hizo ndio za maendeleo na badala yake wanaambiwa imetolewa na rais?

Kuna neno la kigeni linaitwa “deception” (ulaghai, kwa tafsiri isiyo rasmi). Je, tukubali kwamba wananchi wanalaghaiwa kuhusu kodi yao?

Mtu atasema rais anakopa pesa, hivyo akiipata anaitoa kwa wananchi kwa maendeleo yao. Kama hoja ni hiyo, je rais anakopa kwa jina lake au jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Kingine ni kwamba nani atalipa mikopo hiyo kama siyo kodi za wananchi? Wananchi wanajua kwamba wao ndio watakoalipa mikopo hiyo? Mambo



Rais Samia Suluhu Hassan

hayo wapigakura wanayajua? Na je, wanaelezwa?

Kama wapigakura wanaweza kulaghaiwa kwa kodi yao wenyewe, itakuwaje katika upigaji kura wao? Wataweza kuwa na uchaguzi wa busara? Je, kuna haja ya kutafiti uelewa wa wananchi katika mambo ya kawaida kama majukumu ya rais, bunge na serikali?

Je, kama uwelewa wa wananchi ni huo wa kuambiwa “wamepeva pesa zao wenyewe,” wataweza kuhoji matumizi ya pesa hizo? Nini kifanyike, tujadili.

“Hatutaki utalii wa ngono”



Mtalii akiwa na kijana wa Gambia waktvinjari ufukweni.
(Picha kutoka Travelling Jezebel)

BODI ya Utalii nchini Gambia imeziomba nchi zinazopeleka watalii wengi nchini humo kuhimiza utalii wa kujifunza na kufurahi na siyo “ule wa ngono.”

Taarifa iliyotolewa na bodi hiyo wiki iliyopita kwenda serikali za Uingereza, Marekani na nchi zingine, inaeleza kwamba Serikali ya The Gambia haifurahishwi na tabia iliyokomaa mizizi sasa kwa watalii wengi wanaotembelea nchi hiyo ya Afrika magharibi kutafuta vijana ‘mashababi’ kwa ajili ya kufanya ngono.

“Serikali za wenzetu zitusaaidie, watalii wanaotoka huko waelezwe maana ya utalii, siyo kuja kutembea kwetu kwa lengo la kusaka vijana kwa ajili ya kufanya ngono,” ilisomeka sehemu ya barua ya bodi hiyo.

Inadaiwa kuwa kutokana na vikongwe wengi wanaotoka Ulaya na Bara la Amerika, kutembelea The Gambia kwa ajili ya kupata ngono, vijana wengo hawatafuti kazi, bali kusubiri wazee kutoka Ulaya na Marekani.

Telegraph (The Gambia)

Kabuga sasa Kushtakiwa

The Hague
BAADA ya Mahakama ya Makosa ya Uhalifu ya Umoja wa Mataifa (ICC) kutupilia mbali maombi wa kuachiwa huru kwa Felicien Kabuga, sasa atashitakiwa jijini The Hague, Uholanzi.

Kabuga anayedaiwa kuwa kiongozi wa mipango ya mauaji ya halaiki nchini Rwanda ya 1994, atapandishwa kizimbani Septemba 29. Ushahidi utaanza kutolewa Oktoba 5, 2022.

Inadaiwa kuwa Kabuga (80), raia wa Rwanda anayetajwa kuwa tajiri zaidi (wakati huo), alikamatwa nchini Ufaransa Mei 2020 na kupelekwa The Hague, akituhumiwa kuchangia kuibuka kwa mauaji hayo.

Awali, baada ya kukamatwa, mawakili wa Kabuga waliomba mahakama kumwachia huru mteja wao kwa madai ya kuwa na afya iliyodorora.

-Mashirika (Rwanda)

Covid-19 bado kizungumkuti

JANGA la ugonjwa wa Covid-19, siyo kwamba limeacha simanzi na vifo, lakini pia limekuwa chanzo kikubwa cha magonjwa mengine.

Taarifa iliyotolewa mwishoni mwa wiki iliyopita Jijini Johannesburg, Afrika Kusini, zinaeleza kuwa Covid-19 imechochea kuongezeka kwa magonjwa ya moyo, kichaa na sonona.

Chama cha madaktari nchini humo katika taarifa yake kimesema idadi ya wagonjwa wenye matatizo hayo, imeongezeka kwa kiasi kikubwa, sababu ikiwa ni kuwepo kwa janga la ugonjwa huo.

Mail & Guardian (Afrika Kusini)



Pambazuko
Tuko tayari
Kuhesabiwa
kesho,
wewe
je?



Amali ya mtu ni tabia

Na Askofu Dkt. Stephen Munga

WIKI iliyopita mkazo ulikuwa kwamba watu wenye sifa hawapatikani kwa bahati. Upo usemi kwamba mtu ni tabia. Kwa hiyo, watu hutengenezeka kwa kujengewa tabia.

Ina maana kwamba jamii inaweza kutengeneza watu wenye tabia njema au wenye tabia mbaya. Hivyo nirudie kusema tabia ni jumla ya ubora (qualities) na sifa za mtu zinazomtofautisha na watu wengine.

Mpango mzima wa malezi na makuzi yanalenga katika kutengeneza watu. Ni watu wa namna gani inategemea malengo na mpango mzima wa malezi.

Aristotle Nicomachus, mwanafalsafa wa Ugiriki, aliwahi kusema kwamba sifa za mtu hujengeka kwa yale anayojifunza na hujijengea tabia na mazoea kutoka kwa wazazi au walezi na jamii. Kwa hiyo, basi wazazi au walezi wazuri na jamii nzuri hutengeneza watu wazuri au vinginevyo kinyume chake.

Ni mfano wa jinsi mtoto anapoanza kufundishwa kupiga ngoma akifunzwa na mwalimu; na kwamba kadiri siku zinavyokwenda ndivyo maendeleo yake huonekana na vilevile huonekana tabia na uwezo wa mwalimu wake.

Mtu akifikia utu uzima, ana uhuru wa kuchagua kuwa na tabia njema au mbaya. Ikiwa wazazi au walezi na jamii hawana misingi na taratibu nzuri za malezi, basi itatengeneza watu wasiokuwa wazuri. Kwa hiyo, likifanyika kosa la malezi katika kizazi kimoja na kutengeneza watu wasio bora, hakika kizazi kinachofuata baada ya hicho nacho kitabomolewa.

Zaidi ya hayo, kizazi kibovu hakitengenezi kizazi kibovu tu, bali pia hakiwajengeji kizazi kipya uwezo wa uchaguzi mzuri juu ya tabia zao. Inahitajika tabia nzuri kujenga tabia nzuri. Nini kifanyike ili kufanikisha mpango wa utengenezaji wa watu wenye tabia nzuri?

Jamii isipokuwa na utaratibu mzuri



Tabia njema huanza kujengwa tangu utotoni (Picha ya Bezzia.com)

wa malezi, basi kupata watu bora hubaki kuwa kwa kubahatisha. Eneo la malezi ni eneo ambalo linahitaji kufuatiliwa kwa karibu sana.

Ndipo hapo ambapo utafiti na tathmini za dhati juu ya maendeleo ya vizazi na jamii vinahitajika ili kupata taarifa sahihi za kuwzesha utengenezaji wa sheria, sera na mipango ya malezi bora.

Hii ina maana ufuatiliaji wa maisha na hali za familia, makuzi ya watoto na vijana; maendeleo katika mfumo mzima wa elimu na utaalamishaji; uwekaji wa vipimo na viwango vinavyokusudiwa kufikiwa na mipango yake; kupima na kuboresha uhusiano kati ya malezi ya familia na mifumo ya uelimashaji; na uhakiki wa tabia na uwezo wa wadau wote katika taasisi husika.

Mchakato huo ni muhimu kwani waundaji wa falsafa nzuri za siasa na uongozi bora hupatikana kutokana na kundi pana la watu.

Iwapo kundi hilo la watu halina ubora kutokana na maandalizi mavovu, itawezekana kujihakikishia kupata wasukaji wa mifumo safi na ya dhati ya siasa na uongozi? Tafakari!



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mezani kwa Chahali

Anguko la Raila, ushindi wa Ruto

HATIMAYE uchaguzi mkuu wa Kenya ulifanyika Jumanne iliyopita – Agosti 9, ambapo William Ruto, mgombea kwa tiketi ya Kenya Kwanza, alifanikiwa kumshinda mpinzani wake mkuu, Raila Odinga wa Azimio la Umoja.

Lakini, kabla ya kujadili kuhusu matokeo hayo, nitumie fursa hii kuomba radhi kutokana na ubashiri wangu kwenye toleo lililopita la gazeti hili – kwamba Raila angeshinda – kwenda kinyume.

Kama nilivyotanabaisha katika makala husika, moja ya sababu zilizofanyia nibashiri kuwa Raila angeshinda ni kuungwa mkono na rais anayemaliza muda wake, Uhuru Kenyatta. Mara nyingi katika uchaguzi duniani, hususan barani Afrika, mgombea anayeungwa mkono na uongozi uliopo madarakani, hubeba nafasi kubwa ya kushinda.

Sababu nyingine ni ukweli kwamba kura nyingi za maoni zilionyeshwa kuwa Raila akiwa katika nafasi nzuri ya kumbwaga Ruto. Pamoja na kutokuwa sahihi mara zote, kura za maoni zinaendelea kuwa kipimo muhimu katika kubashiri matokeo ya uchaguzi.

Je, kwanini Raila amebwagwa na Ruto katika uchaguzi huo? Nafasi iliyopo kwenye makala hii haitoshi kutaja sababu zote kwa kirefu na badala yake nitataja sababu kuu tu.

Ya kwanza ni kile Waingereza wanaitwa “law of unintended consequences” yaani ofananya hili kwa matarajio haya, lakini matokeo yanakuwa kinyume. Wakati Raila kuungwa mkono na Uhuru kulitarajiwa kumuongezea fursa ya ushindi, inaonekana kuwa suala hilo limeathiri nafasi yake ya ushindi.

Ikumbukwe kuwa kama Uhuru anayetoka ukoo maarufu wa Kenyatta, Raila naye anatoka ukoo maarufu wa Odinga, na koo zote mbili zinaangaliwa na kizazi cha sasa kama himaya zilizotawala siasa za Kenya muda mrefu. Kwa upande



William Ruto, Rais-mteule wa Kenya (Picha ya DN)

wake, Ruto hakuwa na “kasoro” hii.

Pia idadi ndogo ya waliojiandikisha kupiga kura katika maeneo ya kabila la Waluo (la Raila) yalimwathiri mgombea huyo.

Kadhalika, mchakato wa kupata wagombea kwa tiketi ya Azimio la Umoja kwenye nafasi mbalimbali unadaiwa kugubikwa na tuhuma za rushwa na uonevu, kudhani kwamba Ruto alinufaika na “kura za hasira dhidi ya Raila” kutoka kwa waliokerwa na mchakato huo.

Kwa upande mwingine, Ruto alifanikiwa kunadi vyema ujumbe wake wa “taifa la wahangaikaji” (hustler nation) licha ya ukweli kuwa mwanasiasa huyo ni tajiri mkubwa. Mara nyingi tu, katika siasa, ujumbe wa mgombea unaweza kuwa na mvuto kuliko wasifu wake.

Vilevile, kwa mara ya kwanza katika uchaguzi Kenya, ukabila haukuwa na nguvu ya kutosha kumnufaisha Raila, ambaye “mpiga debe wake mkuu” Uhuru anatoka kabila kubwa zaidi la Wakikuyu au kumwathiri Ruto anayetoka kabila dogo la Wakalenjin.

Badala yake Ruto alipata kura nyingi katika ukanda wa Kati ambapo kuna Wakikuyu wengi.

Tanzania yadhibiti magaidi

Na Waandishi Wetu

HOFU iliyokuwa imetanda nchini Tanzania ya kuvamiwa na magaidi walioweka kambi Msumbiji, sasa imetoweka baada ya vikosi maalum kufanya kazi iliyotukuka.

Vikosi maalum vya majeshi na idara zingine za Tanzania viliweka kambi katika mipaka yote inayopakana na Msumbiji na maeneo mengine ya kimbakati, ili kuhakikisha usalama unakuwepo.

Kufuatia matukio ya kigaidi; kuteka, kutesa, kubaka na kuuwa yaliyokuwa yakitokea vijiji vya Jimbo la Jimbo Cabo Delgado, jirani na maeneo ya Mkoa wa Mtwara, Tanzania - magaidi hao walisisika wakitamani "kuvuruga" amani ya Tanzania.

Taarifa za kiintelijensia pia ziliifika Tanzania kuwepo kwa nia hiyo ovu ya magaidi kuingia katika ardhi ya nchi hiyo na kufanya mauaji na pia kupora mali za wananchi.

Inaelezwa kwamba magaidi hao wanaoaminika kufadhiliwa na baadhi ya nchi na makundi mengine ya watu wenye ukwasi kwa malengo yaliyojificha; kubwa ikidaiwa ni kulinda uchochoro wa kupitisha silaha, dawa za kulevya na madini yaliyoporwa.

Kundi hilo la kigaidi, lililoingia Msumbiji mwaka 2017 - lilianza kupata nguvu kwa kupiga baadhi ya vikosi vya Msumbiji na kujiaminisha kwamba linaweza kuongeza eneo kubwa la "kutawala," na siyo Cabo Delgado pekee.

Hata hivyo, baadaye Msumbiji iliomba msaada wa majeshi ya kulinda amani ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na kupunguza nguvu ya magaidi hao. Tayari kundi hilo linadaiwa kuua watu wanaofikia 3,700 hadi sasa.

Pambazuko lililotebelelea Kijiji cha Kitaya, Mtwara wiki iliyopita, limeshuhudia shughuli za kilimo na biashara, zikiendelea bila hofu tofauti na

mwanzoni mwa 2021.

Idadi kubwa ya watu walioulizwa kuhusu wasiwasi wa kushambuliwa na magaidi kutokea Msumbiji, walisema hali kwa sasa ni shwari na hawana hofu tena.

Julius Mang'anya, mfanyabiashara wa korosho katika eneo la Dindwa anaeleza; "hatuna hofu tena, tunaendelea na shughuli zetu na kwa kweli Tanzania ya amani tunaiona hapa, awali hali ilikuwa tete, tulikuwa tunakimbia ili kujiokoa kila mara, hasa nyakati za usiku kwa kuogopa magaidi."

Mchuuzi wa korosho katika eneo hilo, Gideon Limbanga anashukuru majeshi ya Tanzania kwa namna yalivyojipanga kupambana na ugaidi uliokuwa tishio Mtwara na miko mingine jirani.

Anasema wananchi wengi wa Wilaya ya Mtwara waliishi kwa hofu na hawawakuwa na amani. Kwamba milio ya risasi na mabomu ilisikika kila mara na kuleta taharuki kwa watu wengi.

"Hapa kaka ilikuwa hekaheka, watu wengine walihama miji yao, kwa sababu ya hofu ya hawa magaidi, lakini majeshi yetu yalipoweka kambi, amani na utulivu ulirejea na kazi zetu ziliendelea kama kawaida - hadi sasa tuko vyema," anaongeza Limbanga.

Kwanini Msumbiji ilishindwa

Pambazuko limeelezwa na baadhi ya maofisa usalama kwamba majeshi ya Msumbiji yalishindwa kuwadhibiti magaidi kutokana na sababu kubwa mbili.

Moja ya sababu ni baadhi ya makamanda wa Jeshi la Msumbiji kugubikwa kwa ufisadi uliopitiliza kwa kuajiri wanajeshi hewa (ghost soldiers) 7,000 waliokuwa wakipokea mishahara na stahiki zingine kila mwezi.

"Hili liligundulika baadaye wakati majeshi ya nchi za SADC yalipofika kusaidia operesheni hiyo, sasa walipotakiwa askari, wa kutosha,

Tanzania yadhibiti magaidi

hawakuwepo, ni hatari sana,” amesema kamanda mmoja aliyekataa kutajwa jina lake gazetini.

Sababu nyingine ni wanajeshi kuamua kuuza silaha zilizokuwapo kambini na kwenye vituo vya Polisi na kuwapa vijana ambao baadaye walijiunga na magaidi.

EU yaongeza nguvu

Katika kusaidia “kuwamaliza” magaidi nchini Msumbiji, Umoja wa Ulaya (EU) unapanga kuongeza kwa zaidi ya mara tano msaada wa kifedha kwa jeshi la SADC kuimarisha operesheni hiyo.

Pambazuko limeona waraka wa EU kwenda SADC ambao unaeleza kinagaubaga sababu za ongezeko hilo la fedha; kwamba ni kuwaseta magaidi kutoka ukanda wa jimbo hilo lenye utajiri mkubwa wa gesi, mafuta na madini.

Gazeti hili pia limeona taarifa inayoeleza kwamba katika kikao cha SADC kinachoketi wiki hii – Agosti 25 Jijini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), EU itaweka hadharani kiasi cha Dola za Marekani 15.3 kwa ajili ya kuukabili ugaidi Msumbiji.

Msaada huu ni kwa ajili ya kupambana na mashambulizi ya makundi ya kigaidi yanayotishia miradi ya gesi na mafuta nchini Msumbiji.

Mchambuzi wa masuala ya amani Afrika, Kakwesi Abdiei kutoka Nairobi, Kenya ameliambia Pambazuko kwamba msaada huo wa EU unalenga kuhakikisha gesi ya kutosha kwa nchi za umoja huo.

“Pamoja na kwamba ni jambo jema kupata msaada kukabili ugaidi, lakini ukweli ni kwamba nchi za Ulaya na Marekani, zina hali ngumu ya uhakika wa gesi, baada ya kuwepo kwa vita ya Russia na Ukraine,” anasema.

Msmo huyo anabainisha kuwa magaidi wa Msumbiji wataondolewa na kumalizwa kabisa, lakini kutaibuka maswali mengi endapo EU na nchi zingine zinazotarajiwa kuvuna gesi ya Msumbiji, kama zitakuwa na “uhusiano

wa kibiashara wenye tija baina ya Msumbiji na nchi hizo.”

Anasema vita vya Russia na Ukraine vimeongeza msukumo katika mapambano ya nchi za Ulaya kutafuta gesi kwenye pwani ya kaskazini mwa Msumbiji, ambapo kampuni za mafuta za nchi tajiri za Ulaya na Marekani zimepanga kujenga vituo na mitambo ya kuvuna kiasi kikubwa cha gesi asilia inayomiminika kutoka Msumbiji.

Wachambuzi wengine wameliambia Pambazuko kwamba hatua ya EU kusaidia mapambano dhidi ya ugaidi Msumbiji inakuja wakati nchi za umoja huo zikitaka kukabiliana na ushawishi wa China katika rasilimali za Msumbiji.

Msumbiji ina hifadhi kubwa ya gesi ambayo ya tatu kwa ukubwa barani Afrika, baada ya Nigeria na Algeria.

Umoja wa Ulaya unahofia kwamba bila ya kuungwa mkono na kuingilia kati kijeshi, Msumbiji inaweza tena kupoteza udhibiti wa eneo la kaskazini kwa magaidi.

Kampuni zafika Msumbiji

Kampuni ya TotalEnergies ya Ufaransa ambayo imewekeza kiasi kikubwa cha fedha katika mradi wa gesi na mafuta Msumbiji, pamoja na kusimamisha shughuli zake kutokana na mashambulio ya kigaidi Msumbiji mapema mwaka 2021, bado inapanga kuanza uzalishaji mnamo 2024 kutoka kwa akiba kubwa ya gesi inayokadiriwa kuwa na futi za ujazo kwa matrilioni.

Halafu ipo kampuni ya mafuta ya Italia ya ENI ambayo inatarajia kuanza usafirishaji wa gesi kutoka eneo la pwani ya Msumbiji mwaka huu.

Pia kuna kampuni nyingine kubwa ya mafuta na gesi ambayo inaendelea kuwekeza katika ardhi ya Msumbiji kwa lengo la kupata nishati ya uhakika. Kampuni hiyo ni ExxonMobil ya Marekani.

Hivi Tanzania inakwama wapi kukabili ufukara?

Na Godwin Chilewa, Texas, Marekani

“HALI ya maisha ni ngumu sana” Haya ndiyo maneno yanayotajwa kila siku, na pengine mara nyingi, kuliko maneno mengine yoyote kwa sasa.

Kila mahali utakapokwenda, utasikia watu wakilalamikia ugumu wa maisha. Tena, tofauti na zamani ambapo waliokuwa wakilalamika ni watu wa kipato cha chini tu, siku hizi hata wafanyabiashara wakubwa, watumishi wa serikali, na hata viongozi wenye nyadhifa kubwa - nao wanalalamika.

Hivi karibuni nilizungumza na jamaa yangu, mtumishi wa serikali, nilipomwambia kuwa hali ya maisha ni ngumu mno, yeye alikataa katakata! Akasema huyo aliyekwambia hali ni ngumu kakudanganya.

Nilipomuuliza ana maana gani, aliniambia hali ya maisha siyo ngumu, ni mbaya! Aliongeza kusema kwamba kule kutumia neno ‘hali ni ngumu’ ni kupunguza uzito wa hali halisi.

Kwa ujumla hali ngumu ya maisha haiikabili Tanzania peke yake, nchi nyingi duniani, ikiwa pamoja na mataifa makubwa kama Marekani, Uingereza na mengine, yanakabiliwa na changamoto hiyo.

Vita kati ya Russia dhidi ya Ukraine vimesababisha kupanda kwa bei ya mafuta ya kuendesha mitambo na bidhaa nyingine, mabadiliko ya tabia-nchi, yamesababisha kupungua kwa uzalishaji wa chakula na bidhaa za biashara. Pia janga la Covid-19, nalo limesababisha matatizo mengine makubwa ya kijamii na uchumi.

Hivyo, kimsingi mtu mwenye akili timamu havezi kuilaumu serikali



Hali ya ufukara inawesa kutafsiriwa kwa picha hii. (Picha ya mtandao).

ya Tanzania kwa kuwa chanzo cha matatizo yaliyopo, wananchi wanayo kila sababu ya kutathimini na kuhoji mipango na hatua zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na serikali katika kupambana na majanga ili kuwapa ahueni ya maisha wananchi.

Pengine changamoto kubwa inayoikabili Tanzania pamoja na nchi nyingine nyingi za Afrika ni kutokuwa na mipango thabiti, na ya muda mrefu, inayolenga kujihami kiuchumi nyakati za majanga.

Udhaifu huu umesababisha wananchi kuumia kila gharama za maisha zinapopanda na maradufu pale uchumi wa dunia unapoyumba.

Mbaya zaidi ni kuwa mambo yanapokuwa magumu, serikali hugeuka kuwakamua zaidi wananchi kwa kodi, tozo na ushuru badala ya kuwapa ruzuku ya kuwasaidia kupunguza makali ya ugumu wa maisha.

Ufukara na uchumi wa bluu

Na Mwandishi Wetu, Zanzibar

BABA wa uhuru wa Zanzibar, Abeid Amani Karume alikuwa na ndoto ya kuifanya Zanzibar kuwa na maendeleo na hali ya maisha ya watu wake yenye kufikia viwango vya nchi za Ulaya.

Aliyasema hayo mara kwa mara; iwe katika mikutano ya ndani ya viongozi wa serikali au kwa umma anapohutubia. Aliamini katika maendeleo ya taifa kuletwa kwa juhudi za wananchi na mipango mizuri ya serikali.

Hakuyasema haya bila kuonyesha vitendo. Alipambana kukusanya kodi na kuwa na matumizi bora ya fedha za umma. Aliweka akiba na kamwe hakutapanya makusanyo kwa kununua anasa – kuwa na magari ya kifahari ya serikali au kuwekeza kwa viongozi badala ya wananchi.


Sheikh Karume (sasa marehemu) kutokana na hulka yake ya kuangalia zaidi wananchi, hakuiba. Aliweka akiba ya fedha za kigeni hata kufikia kukopesha Tanganyika.

Viongozi wote wa Zanzibar waliopita – inadaikiwa juhudi zao zikijumuishwa pamoja, bado haziwezi kuakisi maendeleo yaliyofanywa na Karume kwa kipindi cha miaka tisa, kuanzia 1964 hadi alipouawa mwaka 1972.

Itoshe tu kusema kwamba Rais Karume alikuwa na maono kwamba Zanzibar inaweza kabisa kuchomoza na kuwa mfadhili wan chi jirani kwa kuwa imezungukwa na rasilimali nyingi.

Visiwa vya Zanzibar ni miongoni mwa maeneo ya Afrika ambayo yanajenga ukanda wa ufukweni wa kilomita 31,000. Ikiwa ni sehemu muhimu kwa ajili ya kuendesha biashara.

Eneo hili la ufukwe linafaa kwa uchumi wa bluu. Hii ni aina ya uchumi ambao unalenga katika matumizi bora – na yenye faida, ya bahari pamoja na rasilimali zake



Rais Abeid Amani Karume

katika kuchochea maendeleo.

Na uchumi huu hutegemea sana ufanisi wa sekta za utalii kwani zaidi ya asilimia 50 ya watalii duniani hutembelea nchi za fukwe.

Kwa sababu hii, ndani ya dira ya maendeleo kuelekea mwaka 2050, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imetamka kwamba uchumi wa bluu utakuwa ndio uti wa mgongo wa mipango yake ya maendeleo.

Dira hii imelenga kuifikisha Zanzibar kwenye nusu ya pili ya uchumi wa kati, yaani “upper-middle income status” na kuwa mwanga wa kupunguza ufukara kwa watu wa visiwa hivyo.

Jiografia na eneo la Zanzibar haliwezi kukidhi mahitaji ya makazi ya watu pamoja na ardhi kwa ajili ya shughuli kubwa za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji na viwanda, hivyo njia nzuri ya kutumia ardhi kidogo iliyopo, huku nguvu kubwa ikielekzwa kwenye matumizi ya maji. Ni uchumi wa bluu pekee ndiyo utaiweka Zanzibar katika mizania ya uhuru wa kiuchumi.

Kwa utaratibu huo, Zanzibar inaweza kuwa kama Singapore ya Afrika, lakini, ni lazima watu wawajibike, kila mmoja kwa nafasi yake, huku serikali ikikusanya kodi stahiki na kuwa na matumizi yenye tija, siyo anasa kwa viongozi wakuu.

Tutakumbuka Daima...



Muasisi na Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, akimfariji mjane wa aliyekuwa Rais wa Msumbiji, Graca Simbine Machel, baada ya mumewe, Samora Machel kufariki dunia katika ajali ya ndege iliyotokea Oktoba 19, 1986. Mwalimu (sasa marehemu) alikwenda Msumbiji kushiriki msiba huo. (Picha kutoka Maktaba ya Pambazuko).

Ngeli za Nomino



Na Dkt. Michael Mashauri

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

M/MI noun class

Leo tutazungumzia juu ya ngeli za nomino (Noun Classes) hujumuisha majina ya mimea mingi, baadhi ya viungo vya mwili na majina mengine. Viambishi vyake vya umoja ni M- na wingi ni MI-.

Hata hivyo, kuna baadhi ya nomino huwa na viambishi vya umoja MW- au MU. MW- hujitokeza ikiwa shina la nomino limeanza na irabu (a, e, i au o) na ikiwa shina linaanza na irabu /u/ au kiyeyusho /w/ huchukua MU.

(This noun class includes most of plant names, some body parts and other names. Its prefixes are M- singular and MI- plural. However, there are some nouns which have MW- or MU- for singular. When the stem begins with vowel (a, e, i or o) it takes MW- and if the stem begins with the vowel /u/ or glide /w/ it takes MU).

Examples:

Prefixes		Class	Root	Examples		English translation
Singular	Plural			Singular	Plural	
m-	mi-	m-/mi	-li	mti	miti	tree/trees
m-	mi-		-guu	mguu	miguu	leg/legs
m-	mi-		-papai	mpapai	mipapai	pawpaw tree/pawpaw trees
mw-	mi-		-ili	mwili	mili	body/bodies
mw-	mi		-ezi	mwezi	miezi	month/months
mu-	mi-	-wa	muwa	miwa	sugarcane	

Ø/JI/MA noun class

Ngeli hii hujumuisha majina ya matunda, baadhi ya sehemu za mwili na majina mengine. Katika umoja huwa na kapa kwa majina mengi au kiambishi JI- kwa baadhi ya majina na katika wingi ni MA-.


(This noun class consists of fruits' names, some body parts and other names. In singular, it takes null prefix for many names or prefix JI- for few names and MA- for plural.)

Examples:

Prefixes		Class	Root	Examples		English translation
Singular	Plural			Singular	Plural	
ji-	ma-	Ø/ji-/mi	-cho	jicho	macho	eye/eyes
ji-	ma-		-we	jwe	mawe	stone/stones
Ø-	ma-		nanasi	nanasi	mananasi	pineapple/pineapples
Ø-	ma		yai	yai	mayai	egg/eggs
Ø-	ma		jambo	jambo	mambo	an issue/issues

Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kuzima intaneti ni kuminya haki za binadamu



Na Simon Mkina

MARA zote serikali zenye kuongozwa na watawala dhalimu duniani, huzima mtandao wa intaneti kwa madai makubwa matano; kuimarisha usalama wa taifa, kulinda uchaguzi, kuepusha vurugu, kuzuia udanganyifu kwenye mitihani na kukwamisha kusambaa kwa taarifa za uzushi.

Hata hivyo, madai yote haya hutolewa kwa sababu ya woga wa serikali hizo dhidi ya nguvu ya umma, kwani wananchi wanapogundua kudanganywa, kutendewa uonevu na serikali iliyoko madarakani uhofia uhai wake, hivyo njia rahisi ya kudhibiti nguvu hiyo ni kuwanyima mawasiliano na taarifa.

Ifahamike kuwa, katika dunia ya sasa, serikali dhalimu huogopa zaidi umma wenye kuwasiliana na kuwa na sauti moja yenye nguvu. Serikali nyingi hazitaki umma wenye taarifa sahihi; zinapenda watu wake wapate taarifa 'zilizochujwa' ama zisizokuwa sahihi na 'nusu-nusu.'

Madai haya ya serikali hizo

zinazoongozwa kiimla, yamezoeleka, hasa katika nchi za Pakistan, Indonesia, Iran, Iraq, Jordan, Kazakhstan na Myanmar.

Takwimu za Shirika la Access Now lenye makao yake makuu New York, Marekani linaeleza katika taarifa zake za hivi karibuni - kwamba mwaka 2019 na 2020, ulikuwa mbaya zaidi duniani baada ya nchi 78 kuzima mtandao wa intaneti kwa madai yaliyoainishwa hapa.

Inaelezwa pia kwamba mwaka uliofuata wa 2021, India iliongoza dunia kwa kuzima mtandao wa intaneti mara nyingi zaidi kuliko nchi yoyote. Nchi hiyo inayotajwa kuwa bingwa wa teknolojia, ilizima mtandao huo mara 106, kati ya 182 - iliyoripotiwa kutoka nchi 81.

Kwa mara ya kwanza, Tanzania ikaonekana katika taarifa hiyo ya miaka miwili - 2019 na 2022, ingawa nchi hiyo ilizima mtandao huo na kukaa kimya. Serikali haikutoa madai yoyote kama nchi zingine zinavyofanya. Iliamua kuminya

Kuzima intaneti ni kuminya haki za binadamu

mawasiliano hayo kimyakimya.

Taarifa zinaeleza kuwa kuzimwa kwa mtandao huo nchini Tanzania kulitokana na sababu ya hofu, wakati nchi ikijiandaa na uchaguzi wake mkuu wa mwaka 2020, ambapo nguvu ya upinzani ilionekana kuimarika – tena ikikomazwa na matumizi makubwa ya mtandao wa mawasiliano na upashaji habari.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) wa wakati ule, James Kulaba, alikataa kuweka wazi sababu za kuzimwa kwa mtandao huo.

“TCRA haipo kwa ajili ya kuzuia watu kupata habari na kuwasiliana, bali kutoa fursa kwao kuwa na mtandao wenye uhakika wa intaneti na kuwa chanzo cha kuwaletwa maendeleo,” alisema injinia huyo.

Pamoja na kushindwa kukubali kwamba mtandao wa intaneti ulizimwa mara kadhaa, lakini alikiri kwamba “endapo ilitokea hali hiyo, basi huenda mitambo ilikuwa katika matengenezo kwa muda.”

Intaneti ni haki, ni maisha

Kuzimwa mwa mtandao wa intaneti kwa Tanzania kulileta taharuki, siyo kwa viongozi na wanachama wa vyama vya siasa, kama iliyoielezwa na wachambuzi, bali kuna idadi kubwa ya wananchi ambao walikiri “kuvurugwa kwa maisha” yao.

Wananchi waliohojiwa walidai kuzimwa kwa intaneti kuliathiri mtitiriko wa shughuli zao za kuingiza kipato kila siku, kwani sehemu kubwa ilitegemea kuwepo kwa mawasiliano hayo.

Magayane John (29), msimamizi wa duka la huduma ya intaneti anayefanya shughuli zake eneo la Mwenge, Dar es Salaam, anakiri kwamba kuzimwa kwa mtandao wa intaneti kulimfanya akose mapato kwa siku nzima.

Anasema mapato yake ya Sh. 40,000 hadi 50,000 kwa siku, yalikosekana,

hivyo kuharibu mtiririko wa kipato katika biashara yake. Katika duka hilo, Magayane ana kompyuta 12.

“Licha ya mimi kukosa kipato, lakini wateja wangu, walikosa huduma muhimu, kwani wapo wanaosoma vyuo, wafanyabiashara na watu wa kada mbalimbali wanaotegemea intaneti kufanya shughuli zako,” anaongeza Magayane.

Dkt. Lenny Kasoga, mtaalamu wa uchumi na mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (mstaafu) anaeleza hasara za kuzimwa kwa mtandao wa intaneti ni kubwa zaidi katika dunia ya sasa yenye kutegemea mtandao huo kwa mawasiliano.

Anasema serikali zinazozima mtandao wa intaneti, hazina sababu za maana kufanya hivyo, bali ni kuogopa nguvu ya umma kwa “matendo maovu dhidi yao,” na kwamba ni uonevu tu wa watawala wasiowajibika ipasavyo.

“Ukiangalia kwa umakini, unagundua kuwa madai yote yanayotolewa na watawala kufungia intaneti, ni upuuzi tu, hakuna sababu ya kufanya hivyo; iwe wakati wa uchaguzi au wakati wa amani au kipindi chochote kile,” anaongeza.

Mchumi huyo anasema biashara nyingi za kuagiza na kuuza bidhaa, zinategemea zaidi mawasiliano ya intaneti, yanapozimwa, tafsiri yake ni kuzidisha umasikini kwa wananchi.

Fatuma Karume, wakili wa mahakama kuu na mwanaharakati wa haki za binadamu, akizungumzia kadhaa ya kuzimwa kwa intaneti Tanzania anasema; “ule ulikuwa uhuni wa watawala na kuminya demokrasia.”

Wakili huyo anasema kuzuia intaneti kunaweza kuelezwa kwa maneno machache kwamba –“ni udikteta,” kwani unazuia haki ya msingi ya binadamu, ambayo ni kuwasiliana, kuwa na uhuru wa kujieleza bila kuingiliwa.

Kuzima intaneti ni kuminya haki za binadamu

“Kuzimwa kwa mtandao kunatumwiwa na mataifa dhalimu kuzuia upinzani na kupokonya haki za kuwasiliana - mara nyingi hutumiwa wakati wa vipindi muhimu kama vile uchaguzi au maandamano, lakini kimsingi, wanaoumia ni wengi hata wasiopenda kujihusisha na siasa – ni kinyume cha haki za binadamu,” anasema.

Je, mtu anaweza kuishtaki serikali kwa kufunga intaneti? Fatuma anasema “ndiyo.” Serikali inaweza kushtakiwa mahakamani kwa kuzima intaneti.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, anasema kilichofanywa na serikali wakati ule kilikuwa na dalili mbaya ya uendeshaji wa nchi yenye kujali haki za binadamu.

“Hakukuwa na sababu ya kuzuia watu kuwasiliana na wengine kuendelea na shughuli zao zinazotegemea uwepo wa intaneti ili kufanya kazi na biashara, wengi walikwama kipindi kile na watu walipoteza kipato – haikuwa sahihi hata kidogo,” anasema.

Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Iringa, Lameck Kishimbo anasema kufungwa kwa mtandao wa intaneti hakuathiri wanasiasa pekee, kama serikali nyingi zinavyodhani, lakini ni hakika kwamba huathiri zaidi uchumi wa wafanyabiashara wanaotegemea intaneti.

Lameck ambaye alikuwa mwaka wa pili wakati mtandao wa intaneti unazimwa, akisomea shahada ya kwanza ya sayansi ya kompyuta, anasema wanafunzi wote hutegemea zaidi mtandao huo kupata vitabu na maarifa mengine, unapozimwa, kwa sababu zozote zile, huathiri mwenendo wa masomo yao. Anashauri serikali ya sasa “kuacha hata fikra za kuzima mtandao wa intaneti.”

Je, VPN inasaidia?

Wakati mtandao wa intaneti

unazimwa mwaka 2020, Watanzania walihamasishana zaidi kujiunga na mfumo unaoweza ‘kupiga chenga’ zuiu la matumizi ya intaneti kwenye simu.

Mfumo huo, maarufu kwa jina la VPN, ulihimizwa zaidi na watu wengi wakiwamo wa wanaharakati na wataalamu wa mtandao wa intaneti. Mmoja wao ni mwanaharakati Maria Sarungi ambaye ‘alijitolea’ kuelimisha wananchi njia ya kukwepa zuiu la kupata intaneti.

Akitumia zaidi mtandao wa Twitter, Maria alifundisha namna ya kupakua VPN anuai, huku akieleza manufaa yake, siyo wakati wa kufungwa kwa intaneti tu, bali pia husaidia ‘usalama’ wakati wa kutumia intaneti.

Mtaalamu wa mawasiliano ya intaneti kutoka kampuni ya Microx Solutions ya Jiji la Mwanza, Amrsan Shah anaeleza kwamba VPN ni mfumo wenye uwezo wa kukwepa njia za kufungia mawasiliano ya intaneti kwa kuwa haingii wala kupitia kwa ‘wakala.’

“Ni vigumu sana kuzuia intaneti kwa watu wanaotumia mfumo wa VPN na huenda ndiyo njia sahihi na salama kwa wakati wote kunapokuwa na zuiu la matumizi ya intaneti katika nchi yoyote,” anaongeza.

Peggy Hicks, Mkurugenzi wa Idara ya Ushirikiano, Taratibu Maalum na Haki za Maendeleo, katika Ofisi ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa (OHCHR) anasema - “ukiona serikali zinahangaika kufunga mtandao wa intaneti, anza kutambua kwamba haki za binadamu ziko shakani.

Makala haya ni sehemu ya mpango maalum wa kukusa ujuzi kwa vyombo vya habari unaoendeshwa na Wakfu wa Thomson Reuters. Yaliyoandikwa humu siyo dhamana ya Wakfu.

Prof GC MacCallum na uhuru wa Tanganyika

Na Deusedith Kahangwa

TANGANYIKA ilipata uhuru wake December 9, 1961 – huku ikiwa na kaulimbiu kadhaa za kuhamasisha wananchi kushiriki kujenga nchi yao.

Kaulimbiu zilizotawala kipindi kile ni; “Uhuru na Umoja”, “Uhuru na Kazi” na “Uhuru na Maendeleo.” Hizi zilichochea ushiriki wa wananchi kupigania maendeleo ya nchi yao changa.

Kiunganishi kikuu cha kaulimbiu zote hizo ni neno “uhuru”.

Teleweke kuwa Watanganyika walikuwa na kiu ‘kuu’ ya kuwa huru dhidi ya maadui wa ubinadamu kama vile ujinga, umaskini, maradhi, unyonyaji, utumwa na ukoloni. Hii maana yake ni kwamba walikuwa (na pengine hata sasa bado) wanayo kiu ya kupata elimu, afya bora, kuwepo usawa, na haki ya kujitawala.

Mawazo haya yalitokana na fikra za wanafalsafa maarufu, Profesa Gerald C. MacCallum Jr., wa Marekani, kuhusu maana kamili ya neno “uhuru.”

Wakati watangulizi wake walitofautisha kati ya uhuru-chanya na uhuru-hasi, kama vitu viwili tofauti, Profesa MacCallum aliunganisha dhana hizi mbili na kuongelea pambetatu ya uhuru kama kitu kimoja.

Kupitia makala yake yenye jina la

“Negative and Positive Freedom” ya mwaka 1967, Profesa MacCallum, alifundisha kwamba, tunapoongelea uhuru, tunapaswa kutaja mambo matatu: nani yuko huru, yuko huru dhidi ya vikwazo gani, na yuko huru kufukuzia lengo gani.

Kwa upande mwingine, anachosema Profesa MacCallum ni kuwa, tunapoongelea utumwa, tunapaswa kutaja mambo matatu; nani mtumwa, ni mtumwa kwa sababu ya vikwazo gani, na vikwazo hivyo vinakwamisha ufanisi kwa lengo gani.

Kunaweza kuwepo vikwazo vya kiuchumi kama vile kipato kidogo, kisiasa kama vile ukoloni, kijamii kama vile miiko ya kijamii, kijinsia kama vile mavazi, kielimu kama vile ujinga, kiafya kama vile maradhi, na kisaikolojia kama vile hofu.

Pia kuna vikwazo vya kidini kama vile imani zenye sura ya kishirikina, kiutamaduni kama vile mapokeo ya kichawi, kimaumbile kama vile ulemavu, na kadhalika. Baadhi ya vikwazo viko ndani ya mwili wa mtu wakati vingine viko nje ya mwili wake.

Gerald C. MacCallum Jr. alizaliwa Juni 16, 1925 na kufariki Januari 14, 1997. Alikuwa profesa wa falsafa katika Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madson nchini Marekani.





Vazi rasmi la Mfalme wa Wazulu wa Afrika Kusini, Misuzulu Ka Zwelathini, akiwa katika eneo la Phuga, alikokwenda jana kuapishwa kushika dhamana. (Picha na Ofisi ya Mfalme)

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

